**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

*Dar es Salaam*
*10 Januari, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo amekutana na kufanya mazungumzo rasmi na Mheshimiwa Wang Yi, Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Watu wa China, Ikulu Dar es Salaam.

Rais Dkt. Samia alieleza dhamira ya Tanzania ya kuendeleza ushirikiano wa kimkakati wa muda mrefu na China, na kuishukuru Serikali ya nchi hiyo kwa uhusiano wake wa kudumu na Tanzania.

Halikadhalika, alisisitiza umuhimu wa kupanua wigo wa mauzo ya bidhaa za Tanzania katika soko la China, kuboresha mizania ya biashara na kuendelea kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji pamoja na mahusiano ya kijamii baina ya wananchi wa nchi hizo mbili.

Vilevile, Rais Dkt. Samia alieleza dhamira ya Tanzania ya kufufua na kuimarisha uendeshaji wa reli ya Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), sambamba na kukuza shughuli za kiuchumi zinazotegemea reli hiyo, kwa lengo la kuongeza mchango wake katika maendeleo ya kikanda.

Kwa upande wake, Waziri Wang Yi alisema Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China imedhamiria kuimarisha ushirikiano wake na Tanzania, na kwamba nchi yake inaunga mkono jitihada za maendeleo za Serikali na wananchi wa Tanzania.

Alieleza kuwa TAZARA ni alama muhimu ya historia ya urafiki wa muda mrefu kati ya China na Tanzania, na kwamba China ipo tayari kusaidia maboresho ya reli hiyo ili kuleta ufanisi utakaochangia kikamilifu katika maendeleo ya kiuchumi.



Ikulu Mawasiliano / ikulu_mawasiliano / ikulu_Tanzania / ikulu Tanzania / ikulumawasilano / Ikulu Tanzania / Ikulu Tanzania

Waziri Yi aliongeza kuwa Serikali ya China itaendelea kuwa mshirika muhimu wa Tanzania na kusaidia katika miradi ya kipaumbele, ikiwemo miundombinu, maji, nishati safi ya kupikia, pamoja na mikopo nafuu na misaada ya maendeleo.

Nchi zote mbili zilithibitisha dhamira yao ya pamoja ya kuendeleza uhusiano kati ya China na Tanzania, pamoja na kuendeleza ushirikiano wa kimataifa na wa pande nyingi kwa manufaa ya pamoja.

**MAELEZO KWA MHARIRI**

Thamani ya uwekezaji nchini Tanzania imeongezeka hadi kufikia dola za Marekani bilioni 1.7 za uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni katika mwaka uliopita.

Biashara kati ya Tanzania na China imeendelea kuimarika, ambapo mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda China yaliongezeka kwa takribani asilimia 85 kati ya mwaka 2020 na 2025, huku uagizaji wa bidhaa kutoka China ukiongezeka kwa takribani asilimia 120, hali inayochangiwa na sera za China za kufungua masoko kwa nchi za Afrika.

Shaaban Kissu
Naibu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu